



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI**



*Unapojibu tafadhari taja:*

Kumb. Na.HW/MUF/S.50/19/VOL.X/44

19/08/2020

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa ya kuomba nafasi za ajira ya Utendaji wa Kijiji kwa masharti ya kudumu

### **1. Mtendaji wa Kijiji Daraja III – TGS B (NAFASI – 06)**

#### **(i) Sifa za Mwombaji:**

- Kuajiriwa wenye Cheti cha Mtihani wa Kidato cha IV au sita (VI)
- Aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### **(ii) Kazi za kufanya:**

- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao
- Kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- Katibu wa Mkutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, Umaskini na kuongeza uzalishaji Mali
- Kutafsiri na kusimamia Sera, sheria na taratibu

- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalamu katika Kijiji
- Kupokea na kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi
- Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

**VIGEZO NA MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI:**

- Mwombaji awe raia wa Tanzania.
- Awe na umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18.
- Maombi yote yaambatishwe na nakala ya cheti cha Taaluma, cheti cha Kidato cha Nne na cheti cha kuzaliwa.
- Maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) ikiwa na anuani, namba za simu za kuaminika, majina matatu ya wadhamini na picha mbili (Passport Size) za hivi karibuni
- Vyeti vyote vya Taaluma, kidato cha nne na cheti cha kuzaliwa vithibitishwe na Hakimu/Wakili anayetambulika na Serikali.
- Aidha, uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria na Mamlaka zinazohusika.
- Mwombaji yejote ambaye hatazingatia mojawapo ya masharti au vigezo tajwa hapo juu maombi yake hayatashughulikiwa.
- Watumishi waliopunguzwa kazi/kufukuzwa kazi Serikalini hawaruhusiwi kuomba.
- Maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili/Kiingereza.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 01/09/2020 saa 9.30 alasiri

Barua zote zitumwe kwa:-

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI  
S.L.P. 223, MAFINGA**

Netho N. Ndilito  
**MKURUGENZI MTENDAJI H/WILAYA  
MUFINDI**

Nakala: Mbao za Matangazo

: Tovuti ya Halmashauri